# UTAFUTAJI, UUNDAJI NA UTUMIAJI WA ISTILAHI KATIKA TAFSIRI

**C.M.T. Bwenge**

## Utangulizi

Lengo la makala haya ni kujaribu kudokeza na kujadili pale inapowezekana juu ya matatizo ya kiistilahi katika mchakato wa kutafsiri na jinsi mfasiri anavyoweza kuyatatua. Aidha msisitizo utakuwa kwenye mbinu za utatuzi wa tatizo la kiistilahi ambapo hatua mbalimbali zitajadiliwa kuanzia ubainishaji wa tatizo, utafutaji wa istilahi hadi uundaji wa istilahi na hatimaye utumiaji wake. Kiswahili kitatumika kama mfano wa lugha lengwa (LL) ambapo Kiingereza kitakuwa mfano wa lugha chanzi (LC).

## Dhana ya Istilahi

Suala la istilahi kwa kuhusiana na tafsiri si geni machoni mwa wafasiri wa Kiswahili. Suala hili limekuwa likijadiliwa sana katika semina, warsha, makongamono na mikutano ya kimataifa na kitaifa tokea miaka ya nyuma hadi leo hii. Kwa mfano, suala la matatizo ya istilahi za kisayansi na kiufundi katika kutafsiri matini za nyanja maalum limekuwa likijadiliwa katika mikutano yote ya Shirikisho la Kimataifa la Wafasiri (FIT) kuanzia miaka ya 1950 (*Stoberski* 1981:475). Dhana ya istilahi imefungamana na dhana ya nyanja maalumu katika jumla ya maarifa ya binadamu. Kila uwanja au taaluma ina msamiati wake maalumu unaowakilisha dhana mahususi katika uwanja unaohusika. Kwa hiyo tunaweza kusema kuwa istilahi ni mfumo kwa msamiati maalumu unaotumiwa katika uwanja/taaluma maalumu (ISO/R1087; Krommer-Benz, 1977:1; TUKI,1990). Istilahi yaweza kuwa alama, herufi, neno au kifungu cha maneno. Pia neno istilahi hutumika kwa maana ya taaluma inayoshughulikia nadharia, kanunu, mbinu na miongozo ya uundaji wa istilahi. (TUKI, 1990).

## Dhima ya Istilahi

Dhima ya istilahi kwa jumla ni kufanikisha mawasiliano baina ya watu wote wanaoshiriki katika mawasiliano kuhusu uwanja au taaluma fulani. Maendeleo katika nyanja au taaluma mbalimbali hutegemea sana uwasilishwaji wake ambao hufanikiwa tu iwapo dhana muhimu katika uwanja unaohusika zinafahamika kwa namna moja kwa wale wote wanaohusika (Galiski, 1985:264; Goetschalckx, 1989.41).

Kwa hiyo istilahi kama mfumo wa msamiati maalumu unaotumiwa katika uwanja fulani mahususi ni msingi wa:

(a) Mpangilio madhubuti wa maarifa (mf. uainishaji wa dhana katika kila taaluma ya kisayansi)

(b) ufundishaji wa maarifa, ujuzi na teknolojia (elimu na mafunzo)

(c) uundaji na usambazaji wa taarifa na maarifa yahusuyo taaluma mbalimbali (maandishi na machapisho mbalimbali), na

(d) uhaulishaji wa matini za kisayansi na kiteknolojia katika lugha nyinginezo (tafsiri/ukalimani).

**Uundaji na Utumiaji wa Istilahi**

Kwa hakika wajibu wa kuunda na kukuza istilahi ni wa wataalamu walio katika nyanja zinazohusika, kwa kushirikiana na wanaistilahi na wanaisimu. Galinski (1985) anasisitiza hoja hii kuwa nyenzo hizo za mawasiliano hazina budi zichukuliwe kama mojawapo ya shughuli za utaalamu wao kwa manufaa ya taaluma na jamii zao kwa jumla.

Mfasiri, kwa upande mwingine, ni mtumiaji tu wa istilahi kama atumiavyo msamiati mwingine wa kawaida. Kati ya dhima za istilahi zilizotajwa hapo juu mojawapo ni kuhaulisha maarifa kwa kutafsiri matini za kisayansi na kiteknolojia kutoka lugha moja kwenda nyingine. Dhima hii inathibitisha ukweli kwamba mfasiri ni mmojawapo wa watumiaji wakubwa wa istilahi. Kwa hiyo katika sehemu zinazofuatia tunajadili matatizo ya kiistilahi yanayomkabili mfasiri na mbinu anazoweza kutumia kutatua matatizo hayo.

**Matatizo ya Kiistilahi katika tafsiri**

*Ukubwa wa tatizo kwa jumla*

Pamoja na mfasiri kuwa mmojawapo wa watumiaji wakubwa wa istilahi, si wakati wote anapokuwa anatafsiri matini za kisayansi au kiufundi anapata istilahi anazozihitaji na zilizo sahihi papohapo. Kutokuwepo kwa istilahi mbalimbali katika lugha lengwa (LL) au kuwepo kwa istilahi zisizolingana katika lugha chanzi (LC) na lugha lengwa (LL) ni tatizo kubwa la kiistilahi katika shughuli ya kutafsiri. Kwa mfano Goetschalckx (1989:42) analiangalia tatizo hili kwa kutofautisha kati ya nchi zilizoendelea; na nchi zinazoendelea; kwamba tatizo linalowakabili wafasiri walio katika nchi zilizoendelea ni kasi kubwa katika maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia inayosababisha kuzuka au kubuniwa kwa dhana mpya kila kunapokucha ambazo zinadai kuundwa istilahi za kuziwakilisha. Uundaji huu wakati mwingine hufanyika kiholela. Tatizo linalowakabili wafasiri walio katika nchi zinazoendelea ni kwamba kila wakati hujikuta wanahitajika kueleza dhana mpya za kisayansi na kiteknolojia katika matini ya lugha chanzi (LC) kwenda katika lugha zao za kitaifa ambazo hazina istilahi za kueleza dhana hizo. Kwa jumla kasi ya maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia haiwiani na kasi ya maendeleo ya kiistilahi.

Tatizo hili ni la ulimwengu mzima. Ni kutokana na utambuzi wa tatizo hili yimeweza kuundwa vyombo vya kimataifa na kitaifa katika nchi mbalimbali ili kutafuta utatuzi wake. Kwa mfano mwaka 1971 kilianzishwa Kituo cha Kimataifa

cha habari za istilahi. [*The International Information Centre for Terminology - INFOTERM*] huko Vienna, Austria ambacho kilikusudiwa kushirikiana na Kamati ya Kiufundi ya 37 [*Technical Committee 37*] ya Shirika la Kimatifa la Viwango [*International Organization for Standardization* (ISO)]. Pamoja na shughuli nyinginezo, kazi kubwa ya kituo hiki ilikusudiwa iwe kuratibu shughuli za ukuzaji istilahi unaofanyika duniani kote kwa kutoa ushauri kuhusu matumizi ya kanuni na mbinu za istilahi, na leksikografia ya istilahi pamoja na kusanifisha katika utunzaji wa taarifa za istilahi.

**Tatizo la Istilahi katika Kiswahili**

Tatizo la istilahi kwa wafasiri wa Kiswahili linaweza kueleweka kwa kuangalia muhtasari juu ya tatizo la istilahi za Kiswahili kwa jumla kama unavyotolewa na Mwansoko na Tumbo-Masabo (1992) kuwa:

> Ukuzaji wa kudhamiria wa istilahi za Kiswahili ambao umekuwa ukiendelea tokea mwaka 1930 umekuwa ukikabiliwa na matatizo anuwai na hivyo kuufanya usiwe na mafanikio ya kuridhisha. Matatizo hayo yanajumuisha upungufu mkubwa wa istilahi katika takribani nyanja zote za taaluma; mparaganyiko wa baadhi ya istilahi unaosababishwa na misingi potovu na/au isiyotimilifu ya uundaji na usanifishaji wa istilahi...(uk.22).

Kwa kuzingatia hali halisi ya tatizo kama inavyodokezwa hapo juu, katika sehemu inayofuatia tunamwangalia mfasiri kama mchunguzi katika uwanja wa istilahi. Swali linalotafutiwa jibu ni, "je mfasiri wa Kiswahili afanye nini anapokabiliwa na tatizo la kutokuwepo kabisa kwa istilahi fulani au kuwepo kwa istilahi zinazotatanisha katika lugha lengwa anayoshughulikia?"

**Mfasiri kama Mwanaistilahi**

Ni jambo lisilohitaji mjadala kwamba wafsiri wa matini za kisayansi na kiufundi kwa kawaida hutumia muda wao mwingi katika kutafuta istilahi za LL. Njia ambayo hutumiwa na wafasiri walio wengi ni kutafuta istilahi (visawe) katika kamusi thaniya mbalimbali za LC - LL za jumla na maalumu, orodha za misamiati maalumu, kuuliza wataalamu walio katika nyanja zinazohusika na kutafuta vyanzo vingine vyenye taarifa za istilahi zinazohusika. Aidha wanaposhindwa kabisa kupata istilahi kwa njia hii, basi hulazimika kuunda istilahi wanazofikiria zinafaa katika kukamilisha kazi zao. Kwa hiyo utafutaji na hatimaye uundaji wa istilahi ni sehemu halisi ya shughuli za mfasiri. Mchakato wote huu ukizingatiwa kama utafiti mahususi na istilahi linganishi kama Lambert (1981:77) anavyopendekeza, basi ni muhimu uzingatie taratibu mahususi za utafiti. Mfasiri ataweza kutatua

matatizo ya kiistilahi kwa urahisi na uthabiti na bila kuumiza ubongo iwapo atakuwa amejizatiti na mbinu za utafiti wa aina hiyo na misingi ya uundaji kwa istilahi. Katika sehemu ifuatayo tunamwangalia mfasiri kama mchunguzi na muundaji istilahi.

**Mbinu za uchunguzi wa kiistilahi**

*Vifaa*

Awali ya yote mfasiri kama mtafiti wa istilahi hana budi awe na vifaa muhimu vya kufanyia kazi pamoja na marejeo muhimu. Vifaa hivi vinaweza kuwa vinamilikiwa na mfasiri mwenyewe au anajua mahali pa kuvipata au kuviazima pindi anapovihitaji. Vifaa hivi vinaweza kugawanywa katika makundi mawili, yaani

(a) vile vinavyohitajika katika kutafsiri k.v. kinakilishi [photocopying machine], taipureta kinasasauti na kompyuta.

b) vifaa vinavyohitajika katika utafiti k.v. kadi bainishi [*index cards*] mbalimbali k.m. za wateja, wafasiri, marejeo; Mafaili k.m. - mafaili ya nyaraka, watoa taarifa, mafaili ya istilahi na tafsiri zilizokwisha fanywa; simu na *kompyuta iliyounganishwa na kompyuta kubwa.

*Marejeo*

Marejeo pamoja na machapisho na nyaraka ni vitu muhimu katika utafiti wa kiistilahi. Marejeo haya yanajumuisha:

(i) kamusi thaniya (za jumla na maalumu) za LC-LL
(ii) kamusi wahidiya (za jumla na maalumu) za LC na LL
(iii) orodha za misamiati mipya za LC na LL
(iv) orodha za istilahi ambazo hazijasanifiwa za LC na LL
(v) Majarida ya tafsiri
(vi) Machapisho mbalimbali ya LC na LL ya mada inayotafsiriwa.


*Uchunguzi*

Vifaa vilivyotajwa hapo juu ni nyenzo muhimu sana katika uchunguzi na hasa katika hatua za awali za utafiti halisi, na ni msingi wa maamuzi yanayofanywa mwishoni. Uchunguzi huu unaweza kujumuisha hatua kama nne hivi ambazo zinalandana na zile zilizopendekezwa na Lambert (1981:77-85):

(1) Ubainishaji wa istilahi zilizomo katika matini ya LC [*identification of terms*]
(2) utafutaji wa istilahi katika LL [*terminographic search*]
(3) Uchunguzi wa dhana [*conceptual research*]
(4) Uundaji wa istilahi za LL

Uhusiano kati ya hatua hizi unaonyeshwa na kufafanulia zaidi katika mchoro uliopo hapa chini:

Mchoro Na 1: Uhusiano wa hatua na mchakato wa uchunguzi wa kiistilahi



Kwa kiasi kikubwa hatua hizi zinangatia misingi ya nadharia ya istilahi kama ambavyo inaelezwa katika maandishi mbalimbali katika uwanja huu (ISO/TC 37/WG 1; Tumbo, 1982:87-98; Mwansoko, 1989 na Mwansoko na Tumbo-Masabo 1992) ambamo pamoja na mambo mengine inasisitiza sana kuwa:

- uundaji wa istilahi hauna budi uanzie kwenye **dhana** na siyo istilahi;
- **dhana** hizo zielezwe kwa ukamilifu na wazi;
- uhusiano baina ya **dhana** ndio uwe msingi wa uundaji kwa istilahi

Kwa mfano, Tumbo (1982:29) anasisitiza kuwa katika shughuli ya kuunda na kusanifisha istilahi kitu muhimu ni kupata dhana sahihi inayowakilishwa na istilahi katika LC ambapo istilahi katika LL inaweza ikaundwa.

Kwa muhtasari kitu kinachosisitizwa katika nadharia ya istilahi ni:

| Istilahi | DHANA | | Istilahi |
|---|---|---|---|
| (LC) | (LC) | (LL) | (LL) |

Kama mchoro unavyoonyesha hapo juu mchakato huu kutoka istilahi ya LC kwenda katika istilahi ya LL unapitia katika hatua mbalimbali ambazo hatimaye humwezesha mfasiri kutatua tatizo la kiistilahi . Pengine inafaa hapa tuangalie kazi ya kila hatua kwa kina.

HATUA 1: **Ubainishaji wa istilahi katika matini ya LC**

Hii ni hatua ya awali kabisa na inajumuisha shughuli zifuatazo:

(i) kusoma kwa makini matini inayohusika
ili kuweza
- kuelewa ujumbe
- kutambua matini yanahusu mada gani
- kubaini uwanja au nyanja
- kubaini istilahi (na msamiati mgumu)

(ii) kuorodhesha istilahi zilizobainishwa (na ikiwezekana kuziorodhesha kwa utaratibu wa alfabeti)

Mfano: kutoka katika matini iliyoambatishwa (Kiambatisho A) tunaweza kubaini haya yafuatayo

mada : sarufi
uwanja : isimu

na istilahi zilizobainishwa zimeorodheshwa kama ifuatavyo:

- grammatical forms
- morphosyntactic categories
- number
- gender
- tense
- mood
- inflectional languages
- agglutinative languages
- isolating languages
- morphology
- inflection
- derivation

Hatua inayofuatia baada ya kuorodhesha istilahi zilizomo katika matini LC, ni kuorodhesha istilahi za LL. Katika hatua hii mambo mawili yanaweza kutokea, nayo ni kwamba istilahi za LL zinafahamika vizuri kwa mfasiri au baadhi tu zinafahamika vizuri na nyingine hazifahamiki au zinatatanisha. Ikiwa istilahi zinafahamika basi zinaorodheshwa moja kwa moja na shughuli ya kutafsiri matini nzima inaendelea. Hapa tunasema hakuna tatizo la kiistilahi. Lakini kama hazifahamiki au zinatatanisha basi tunasema kuna tatizo la kiistilahi ambalo linatupeleka katika hatua ya pili.

HATUA 2: **Utafutaji wa istilahi za LL**

Katika hatua hii shughuli kubwa ni kupitia katika kamusi thaniya mbalimbali za LC-LL ili kuona kama istilahi zipo.

Vyanzo vya taarifa:

- Kamusi thaniya maalumu za LC-LL za nyanja zinazohusika (inafaa kuanza na kamusi mpya)
- Orodha za misamiati ya LC -LL zilizochapishwa katika majarida
- kadi bainishi za istilahi za mfasiri za LC-LL
- kamusi thaniya za jumla za LC-LL

Mfano: Baada ya kupitia *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (KASAILU) (TUKI 1990), istilahi zilizopatikana ni kama ifuatavyo:

| Istilahi (LC) | Istilahi (kisawe) (LL) |
|---|---|
| grammatical forms | - |
| morphosyntactic categories | - |
| number | - |
| gender | jinsi |
| tense | njeo |
| mood | dhamira |
| inflectional languages | lugha ambishi |
| agglutinative languages | lugha ambishi bainishi |
| isolating languages | lugha tenganishi |
| morphology | mofolojia |
| inflection | uambishaji |
| derivation | unyambuaji |

Tumekuwa na bahati ya kukuta idadi kubwa ya istilahi katika kamusi hii. Istilahi hizi zinaorodheshwa moja kwa moja tayari kutumika katika tafsiri. Lakini tafsiri haiwezi kuanza hadi tumepata visawe vya istilahi tatu zilizobaki, yaani

grammatical forms -
morphosyntactic categories
number

Kama ambavyo imekwishaelezwa hapo juu, tunaweza kupita katika kadi bainishi za istilahi kama zipo, ikishindikana tunapitia katika orodha za misamiati ya Kiingereza - Kiswahili iliyochapishwa katika majarida na machapisho mengine na hata katika kamusi thaniya za jumla za Kiingereza-Kiswahili. Baada ya kupitia katika vyanzo hivyo hatukufanikiwa kupata istilahi hizo. Hali hii inatulazimisha tuingie katika hatua nyingine ya uchunguzi wa dhana zinazowakilishwa na istilahi hizo katika LC. Hatua hii tumeiita Uchunguzi wa dhana.

HATUA 3: **Uchunguzi wa dhana**

Uchunguzi wa kina kuhusu istilahi unaanzia katika hatua hii. Lengo la hatua hii ni kupata maana halisi ya istilahi inayohusika katika LC kwa kuzingatia vipengele muhimu vinavyoashiria dhana. Uchunguzi huu unaweza kujumuisha hatua tatu ndogo ambazo ni:

(a) uchunguzi wa kifasili [*definitional investigation*)
(b) uchunguzi wa mada [*subject matter investigation*]
(c) mahojiano [*interviews*]

(a) **Uchunguzi wa kifasili**

Vyanzo vya aina tatu vinaweza kutumika
- Kamusi wahidiya maalumu za LC
- kamusi wahidiya za jumla za LC
- Orodha za misamiati mipya za LC

Vyanzo hivi vinaweza kutoa orodha kubwa ya fasili na pengine isiwepo hata moja iliyokamili. Hata hivyo fasili mbalimbali zinaweza kukamilishana. Kwa mfano, istilahi ambatani "*grammatical forms*" dhana yake inaweza ikachunguzwa kwa kuchunguza fasili ya maneno yanayoliunda ambapo "*grammatical*" inafasiliwa "-a kisarufi" na "*form*" kama "umbo" ling. "*caustative form*" **umbo sababishi** (KASAILU)

(b) **Uchunguzi wa mada**

Lengo la uchunguzi huu ni kutafuta miktadha inayohusiana ambamo istilahi ya LC inaweza kutokea na kutoa mwanga kuhusu maana yake. Miktadha hii inaweza kufahamika kwa kurejea marejeo yanayoshughulikia jambo kama hilo ambamo istilahi inayohusika inatokea. Hapa ni muhimu mchunguzi awe anaelewa vizuri mazingira, miktadha na uwanja huo pamoja na tanzu zake ili aweze kuelekeza uchunguzi wake katika mwelekeo sahihi.

Vyanzo vya taarifa vinaweza kuwa:
- kamusi wahidiya za LC
- machapisho maalumu ya LC
- Makala maalumu katika majarida ya LC
- Nyaraka maalumu za LC

Kila istilahi inayohusika inapojitokeza hapana budi idondolewe pamoja na muktadha wake na kutaja mahali inapodondolewa.

Kwa mfano, maneno yanayounda istilahi ambatani "*grammatical forms*", yaani "*grammatical*" na "*forms*" pia yameshiriki katika kuunda istilahi ambatani nyingine k.v. "*grammatical category*" ambayo istilahi yake, ni "kategoria ya kisarufi" (TUKI 1990:10)

(c) Iwapo juhudi za kupata dhana ya istilahi ya LC katika hatua zilizotajwa hapo juu hazikuleta jibu mwafaka, basi hatua inayofuata ni kuwahoji watu maalumu. Watu wanaoweza kutoa taarifa za kusaidia kupata dhana ya istilahi ni
- mteja (aliyeleta matini)
- mwandishi (wa matini hiyo)
- mtaalamu (wa uwanja huo)

Iwapo mteja ni mzungumzaji mwenyeji wa LC, basi atakuwa katika nafasi nzuri ya kutoa mwanga kuhusu istilahi inayohusika; kwani anaweza akawa anaelewa ujumbe ambao unatakiwa uifikie hadhira ya LL. Hata hivyo, wakati mwingine mteja anaweza akawa hajui au ni mzungumzaji mzawa tu wa LL. Katika hali kama hiyo mteja anaweza kuombwa amweleze mwandishi wa matini (kama yuko mahali ambako mawasiliano yanaweza kufanyika katika muda mfupi). Njia hii inaweza kusaidia kupata jibu kwa sababu hutokea wakati mwingine waandishi wakajiundia maneno yao au wakashindwa kutumia maneno sahihi katika kuandika. Aidha, mtaalamu (kama yuko karibu) wa uwanja unaohusika anaweza kuombwa kutoa ufafanuzi wa istilahi inayohusika.

Baada ya kupata data yote kuhusiana na dhana ya istilahi inayohusika inafuatia hatua ya mwisho ya kuunda istilahi.

HATUA 4: **Uundaji wa Istilahi**

Uundaji wa istilahi ni mchakato unaodai kuzingatiwa kwa baadhi ya misingi ya jumla na misingi mahususi ya uundaji wa istilahi. Katika hatua zilizotangulia kilichokuwa kinaongoza uchunguzi ni misingi ya jumla inayosisitiza kuwa uundaji wa istilahi lazima uanzie kwenye dhana, na dhana hiyo ielezwe kwa ukamilifu na wazi.

Baada ya dhana kuwa imeeleweka vizuri, hatua inayofuatia ni kuunda istilahi ya kuiwakilisha katika LL. Misingi mahususi ya uundaji istilahi ndiyo inayoongoza mchakato huu.

Waandishi wengi katika uwanja wa istilahi (k.v. Ohly 1981; Tumbo 1982; Goetschalckx 1989; Alvey 1989; Mwansoko na Tumbo-Masabo 1992) wanakubaliana kuwa michakato inayotumiwa katika uundaji wa istilahi ni kutafsiri na kutumia lugha yenyewe kwa minyambuliko, miambatano, miungano, uongezaji au upaji maana mpya kwa maneno yaliyopo, ufupisho na akronimi. Mikopo kutoka lugha nyingine nayo pia imeainishwa kuwa mchakato unaotumiwa sana hususa katika nyanja za sayansi na teknolojia. Aidha uchaguzi wa michakato inayotumiwa zaidi hutegemea muundo wa lugha (Mwansoko na Tumbo-Masabo 1992).

Tukiwa tunazingatia misingi mahususi ya uundaji istilahi za Kiswahili kama inavyopendekezwa na wataalamu mbalimbali wa Kiswahili na kuorodheshwa kwa mpangilio mzuri katika Mwansoko na Tumbo-Masabo (1992:24-26), ingefaa hapa tufafanue michakato itajwayo hapo juu kwa kutumia mifano ya Kiswahili.

(i) kutafsiri - uundaji wa istilahi kwa kutafsiri (tafsiri sisisi) istilahi ya LC k.v. Kiingereza. Aghalabu mpangilio wa maneno huweza kubadilika ili ulingane, na kanuni za kisarufi za LL;

k.m. **umbo sababishi** (isimu) kutokana na,
***causative*** (sababishi) na ***form*** (umbo)

(ii) Mnyumbuliko - ni uundaji wa istilahi kwa kuambatisha viambishi kwenye mzizi au shina la neno: k.m. - **uambishaji** (sarufi) '*inflection*' ambalo limetokana na kuambatisha **u** na **aji** kwenye mzizi **-ambish-**

(iii) Mwambatano - ni uundaji wa istilahi kwa kuambatanisha maneno mawili au zaidi yaliyo huru k.m. **lugha tenganishi** '*isolating language*'

(iv) Muungano - ni uundaji wa istilahi kwa kuunganisha maneno mawili au zaidi,

| | |
|---|---|
| k.m. **elimumisitu** | '*Forestry*' |
| **selifito** | '*rod cells*' |
| **elimunafsi** | '*psychology*' |

(v) Kuongeza au kuyapa maneno maana mpya - ni uundaji wa istilahi kwa kulipa neno lililopo katika msamiati wa kawaida maana ya ziada ambayo inawakilisha dhana mahususi katika uwanja unaohusika k.m. **mfumo** [*system*] (siasa, biolojia) ambalo maana ya kawaida ni hali ya kufungwa.

(vi) Ni uundaji wa istilahi kwa kufupisha maneno yanayotumiwa kwa pamoja kwa kuchukua herufi za mwanzo tu za maneno hayo.

k.m. **UKIMWI** - Upungufu wa Kinga Mwilini
[*AIDS - Acquired Immune Deficiency Syndrome*]

SHIHATA - Shirika la Habari la Tanzania

(vii) Mkopo - ni uundaji wa istilahi kwa njia ya kutohoa istilahi ya lugha chanzi katika lugha lengwa; k.m. **sitoplazimu** [*cytoplasm*] (Biolojia) Kiswahili kimekopa istilahi nyingi kutoka katika Kiingereza.

Aidha utohoaji hujumuisha haya yafuatayo:

- usawazishaji wa mfumo sauti k.v. kuongeza irabu tamati kwenye istilahi zinazoishia na konsonanti - angalia "**u**" iliyoongezwa katika mfano wa hapo juu.

- kuipangua mifuatano ya konsonati iliyo migumu kutamkika katika Kiswahili kwa kuingiza irabu kati yake (ang. Mwansoko na Tumbo - Masabo 1992:29-30)
  k.m. cy/cytoplasm - si/sitoplazimu

- ukopaji wa viambishi
  viambishi vya LC hupewa visawe mahususi

| | | |
|---|---|---|
| k.m. | - ism/capitalism | u - /ubepari |
| | - ism/socialism | u - ujamaa |
| | - logy/biolology | lojia/biolojia |
| | - geo/geology | jio/jiolojia |
| | - lexi/lexicology | leksi/leksikolojia |

- Mpangilio wa istilahi zenye maneno ambatani ulingane na sarufi ya Kiswahili k.m. *nitrous oxide* - **oksidi nitrasi** yaani kivumishi kitokee baada ya nomino.

- Majina mahususi ya watu, nchini, maji n.k. yanapotumika katika istilahi yahifadhiwe katika istilahi za Kiswahili.

  k.m. *Haber process* - mfanyiko tandani wa Haber (Kemia)

- Kulingana na kanuni za ISO, inashauriwa alama za elementi na alama nyingine ziachwe kama zilivyo katika Kiingereza na ziandikwe baada ya elementi au tarakimu

  k.m. Klorini cl [*Chrorine cl*]
  (angalia TUKI : *Kamusi Sanifu ya Biolojia, Fizikia na Kemia*)

Baada ya kupata vidokezo hivyo pengine ingefaa tujaribu kuunda istilahi (visawe) ambazo mpaka sasa tunadaiwa kabla ya kuendelea na shughuli ya kutafsiri matini iliyo kwenye Kiambatisho - A nazo ni:

- grammatical forms
- Morphosyntactic categories
- number

Baada ya kuwa tumeelewa dhana zinazowakilishwa na istilahi hizi na miktadha ambamo sehemu zake zinajitokeza tunaweza kutumia njia au mchakato wa utohoaji kwa baadhi ya istilahi na njia ya kutafsiri kwa istilahi zinazobaki kama ifuatavyo:

grammatical forms - maumbo ya kisarufi
morphosyntactic categories - Kategoria za mofosintaksia
number - idadi

Baada ya istilahi kuundwa ni muhimu iandikwe kwenye kadi bainishi ya istilahi - istilahi ya LC inaandikwa kwanza pamoja na fasili yake na kufuatiwa na istilahi ya LL nayo ikiwa na fasili yake. Pia uwanja unaohusika na istilahi mpya huonyeshwa katika kadi bainishi. Manufaa ya taarifa hizi ni kujenga orodha ya istilahi mpya, kuwa na mwendelezo katika uchunguzi wa istilahi na kupunguza bughudha iwapo mfasiri atakutana na istilahi kama hiyo tena.

**Matumizi ya Istilahi**

Haitoshi tu kupata nyenzo za kazi, bali pia ni muhimu kuzitumia nyenzo hizo kwa ufanisi mkubwa (Abu-Ssaydeh 1991).

Matumizi ya istilahi yanahusu kuijaribisha istilahi ili kuona kama inafaa au inakubaliwa. Kwa vile tafsiri inayohusika inakuwa imelenga hadhira ya wazungumzaji wa LL inashauriwa wataalamu wazungumzaji wa LL watoe kauli ya mwisho juu ya usahihi na ubora wake.

Kisha hatua inayofuatia ni kujaribu kuitumia istilahi hiyo katika tafsiri iliyokusudiwa, yaani tafsiri ya matini inaweza ikatumiwa kuona jinsi gani istilahi hiyo inaingia katika sintaksia na mtindo wa matini ya LL.

**Hitimisho**

Katika utangulizi na katika hitimisho la makala haya neno "kudokeza" au "madokezo" limerudiwarudiwa sana. Hii imefanyika kwa makusudi kabisa ili kusisitiza ukweli kwamba masuala ya istilahi katika tafsiri ni muhimu sana na mapana mno kiasi kwamba utakuwa ni uongo kudai kuwa yamejadiliwa kwa kina katika makala moja. Kwa hakika, mfasiri yeyote na hususa mfasiri wa Kiswahili anapaswa kuwa amejizatiti barabara na misingi ya nadharia ya uundaji wa istilahi ili aweze kufanya kazi yake vizuri zaidi hasa ikizingatiwa kwamba kasi ya maendeleo ya istilahi za Kiswahili ni ndogo mno ikilinganishwa na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia na kasi ya uhaulishwaji wa dhana za nyanja hizo katika jamii ya wazungumzaji wa Kiswahili.

Makala haya yalikusudia kutoa vidokezo tu kuhusu matatizo ya kiistilahi katika kutafsiri. Katika mipaka ya lengo hilo makala yamedokeza kuhusu dhana ya istilahi, dhima ya istilahi kwa jumla na katika tafsiri, ukubwa wa tatizo la istilahi katika uwanja wa tafsiri kwa jumla na katika Kiswahili na hatimaye yamejaribu kuonyesha mfasiri kama mwanaistilahi - pindi anapokabiliwa na tatizo la kiistilahi. Katika kipengee kuhusu mfasiri kama mwanaistilahi, ambacho ndicho kiini cha makala nzima, makala yamejaribu kudokeza juu ya hatua na mbinu za utafiti

mahususi na istilahi wakati mfasiri akiwa katika shughuli ya kutafsiri. Hatua muhimu zilizojadiliwa ni pamoja na ubainishaji wa istilahi (za matini ya LC), utafutaji wa istilahi za LL uchunguzi wa dhana zinazowakilishwa na istilahi na hatimaye uundaji wa istilahi kwa kuzingatia misingi ya jumla na mahususi ya uundaji wa istilahi. Makala yamesisitiza kuwa kwa kufuata hatua hizo, mfasiri huweza kutatua tatizo la kiistilahi bila kuumiza ubongo wake sana au kupoteza muda mwingi; na faida kubwa ni kutoa tafsiri nzuri ambalo huwa ndio lengo kuu la kila mfasiri.

Mintarafu ya ukweli huu, mwandishi wa makala haya anapendekeza kuwa zifanyike kila jitihada za kuandaa semina za ya mafunzo ambazo lengo lake litakuwa ni kuwaongezea ujuzi na kuwafundisha mbinu mbalimbali wafasiri wa Kiswahili kuhusu masuala ya istilahi. Hapana shaka semina ya wiki moja inaweza kutosha kuwapatia misingi ya nadharia ya istilahi ambamo vipengee vifuatavyo vitatiliwa mkazo:

- nadharia ya dhana
- uchambuzi wa kinstaksia na wa kimaana wa istilahi
- utoaji wa fasili
- uhusiano baina ya dhana
- mfumo wa dhana
- uhusiano wa dhana na istilahi
- uundaji wa istilahi
- utata wa istilahi
- michakato ya uundaji istilahi
- leksikografia na kanzi ya maneno/istilahi.

**MAREJEO**

Ab - Ssaydeh, A.F. (1991) "A dictionary for Professional Translators". Katika *Babel* 37/2, 65 - 74.

Alvey J. (1989) "The Anglicization of French (with specific referencee to the financial world and some reference to Spanish)". Katika J, Joly, (Mhariri) *Proceedings of the Second North American Translators Congress.* Washington, D.C.

BAKITA, *Tafsiri Sanifu* 2 - 5 Dar es Salaam, 1976 - 1985

Felber, H.(1985) "Terminology Planning in Countries Lacking Developed Terminologies". Katika H, Buhler (Mh.) *Proceedings of the Xth World Congress of FIT* (Wien: Wilhelm Braumu Iler 273 - 277.

Galinski, C. (1985) "The Role of Terminology - Terminology and Translation". Katika H, Buhler (Mh.) *Proccedings of the Xth Word Congress of FIT* (Wien: Wilhelm Braumuller, 264 - 267.

Goetschalckx, J. "Introduction - Terminology as a Tool". Katika J. Joly (Mh.) *Proccedings of the Second North American Translators Congress* Washington, D.C., 41 - 42

Hartmann, R.R.K.(1989) "Translation Equivalence: A Model of Lexical Appreximation and its Relevance to the Terminological Dictionary". Katika H, Buhler (Mh.) *Proceedings of the Xth World Congress of FIT.* Wien: Wilhelm Braumuller, 286 - 290.

ISO, ISO Recommendation R 1087(1969). *Vocabulary of Terminology* Switzerland.

ISO, ISO/TC 37 /WG 1 (1978) "Principles of Terminology" (1978).

Krommer - Benz, M:(1977) "International Activities in the Area of Standardized Terminology", Waraka wa INFOTERM.

Lambert, J.(1981). A general Approach to specific Research in Comparative Terminology". Katika *Babel* Vol XXVII/2, 77 - 85.

Mwansoko, H.J.M.(1989). "The principles, Methods and Procedures of Swahili Terminology Development in Tanzania A re - examination of Basic Issues". Katika *Journal of Asian and African Studies* 38, 161 - 176.

Mwansoko, H.J.M.(1991). "Joint Translation Project: Some Suggestions of the working procedure", katika *Textcontext* 6, 157 - 161.

Mwansoko, H.J.M na Tumbo-Masabo, Z.(1992) "Kiongozi cha Uundaji Istilahi" za Kiswahili. Dar es Salaam TUKI.

Ohly, R. (1981) "Anisomorphism: The African Case" katika A. Kopezynski; A. Hanftwurcel, E. Karska na L Rywin (Wahr.) *Proceedings of the ixth World Congress of FIT.* Warsaw : PAI, 178 - 180.

Palmer, F.(1971) *Grammar*, London: Penguin Books;

Picht, H.(1985) "The Terminology Component in Translators Training Programmes". Katika H. Buhler (Mhr.) *Proceedings of the Z Xth World Congress of FIT.* Wien : W & B, 1985 338 - 342.

Shaikerich, A na Oubine, I.(1988). "Translators and researchers look at bilingual terminological dictionaries". *Babel* 34/ 1, 10 - 16.

Stoberski, Z.(1981). "World Bank of International Terminology". Katika A. Hanfturcel, E. Karska na L. Rywin (Wahr.) *Proceedings of the ixth World Congress of FIT.* Warsaw : PAI, 425 - 427

TUKI,(1991). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors;

TUKI *Kamusi(1990). Sanifu ya Biolojia, Fizikia na Kemia.* Dar es Salaam : EPD;

Tumbo, Z.(1982) "Towards systematic Terminology Development in Kiswahili *Kiswahili*" 49/1, 87 - 98.

## Kiambatisho - A

**The Morphology of derivation**

The discussion so far has been concerned with variation in closely related grammatical forms of words, involving Morphosyntactic categories such as number, gender, tense and mood. It has necessarily ben limited to inflection features of languages have, by definition no variation, while isolating languages have no morphology. It has been concerned, that is to say, solely with inflection, to the exclusion of derivation. (F. Palmer, **Grammar**, 19:118)

**Mofolojia ya Unyambuaji**

Hadi kufikia hatua hii mjadala huu umezingatia mwachano katika maumbo ya maneno yanayohusiana sana kisarufi. Maumbo haya yanajumuisha kategoria za mofosintaksia kama vile idadi, jinsi, njeo na dhamira. Aidha imebidi mjadala ujifunge katika mipaka ya lugha ambishi (au tuseme katika mipaka ya sifa ambishi za lugha) kwa sababu lugha ambishi bainishi huwa hazina sifa za mwachano, ambapo lugha tenganishi hazina mofolojia. Kwa hiyo mjadala umejihusisha tu na suala la uambishaji na kuacha kando suala la unyambuaji.